



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. BDC/S.20/10/VOL.II/27

05 Novemba, 2021

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa za kuomba nafasi mbili (02) za kazi kwa **Mkataba Fundi Sanifu Ujenzi Daraja la II - TGS C (Civil Technician)**.

1.0 FUNDI SANIFU UJENZI DARAJA LA II -TGS C (Civil Technician) nafasi (02).

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Elimu ya Kidato cha VI na kufuzu mafunzo ya ufundi ya miaka miwili (02) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali katika moja ya fani za ufundi Au awe amehitimu Kidato cha IV na kufuzu kozi ya ufundi ya miaka mitatu (03) kutoka Vyuo vya Ufundi vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani za ufundi Au awe na Cheti cha majaribio ya ufundi hatua ya **I** kutoka Chuo cha Ufundi kinachotambuliwa na Serikali Au awe na Stashahada ya kawaida katika fani za ufundi kutoka Chuo cha Ufundi kinachotambuliwa na Serikali.

1.2 MAJUKUMU

- a) Kuandaa makisio ya vifaa vya ujenzi
- b) Kuandaa michoro ya majengo
- c) Kusimamia kazi za ujenzi kuhakikisha zinakidhi viwango
- d) Kuandaa mpango kazi wa ujenzi
- e) Pamoja na kutekeleza majukumu mengine atakayopangiwa na mwajiri.

1.3 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
2. Awe mwadilifu na asiwe na historia ya uharifu.
3. Waombaji wote waambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa
4. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
5. Picha moja Passport Size iandikwe jina kwa nyuma.
6. Hati za matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (**Statement of Results havitakubalika**)
7. Waombaji waliosoma Nje ya Nchi wahakikishe Vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika.
8. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili na yatumwe **kwa njia ya Posta kabla ya tarehe 18/11/2021 saa 09:30 alasiri** kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 157,
BUSEGA.



Veronica Vicent Sayore
Mkurugenzi Mtendaji

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA.

**MKURUGENZI MTENDAJI
H/ WILAYA YA BUSEGA**